# Je, tunawekeza kwa ufanisi kwenye elimu?

## Kufuatilia Mwenendo wa Ugharamiaji wa Sekta ya Elimu
## Ripoti ya uchambuzi wa bajeti ya mwaka 2014/2015

Agosti 2014

hakielimu

## Shukrani

Uchambuzi na uandishi wa ripoti hii umefanywa na Makumba Mwemezi wa Idara ya Utafiti na Uchambuzi wa Sera HakiElimu. Maelekezo ya kitaalam yametolewa na Godfrey Boniventura na Elizabeth Missokia. Tunawiwa kuwashukuru pia ndugu Robert Mihayo na Presscodd James kwa michango yao ya uhariri, bila michango yao wote muhtasari huu usingekamilika ipasavyo.

@ HAKIELIMU, 2014

ISBN 978-9987-18-043-1

HakiElimu, S.L.B 79401, Dar es Salaam

Simu: (255 22) 2151852/3

Faksi: (255 22) 2152449

Baruapepe: info@hakielimu.org

Tovuti: www.hakielimu.org

Sehemu yoyote katika kitabu hiki inaweza kutolewa kwa namna nyingine yeyote kwa madhumuni ya kielimu na yasiyo ya kibiashara, kwa kuzingatia kuwa chanzo kitatajwa na nakala mbili ziwasilishwe HakiElimu.

## Utangulizi

Kwenye ukurasa wa tovuti yake, Kongamano la Uchumi Duniani (GES) limeandika kuwa; "Kuwekeza katika elimu halijawahi kuwa jambo ghali zaidi, ingawa lina gharama zake kila mahali lakini jambo lenye gharama kubwa zaidi ni kuacha kuwekeza kabisa. Uwekezaji duni kwenye elimu unaongeza gharama kubwa kwa jamii katika masuala ya ugharamiaji wa matumizi ya umma, uhalifu, afya, na ukuaji wa uchumi."

Elimu ni haki ya msingi kwa kila mtu na muhimu kwa mustakabali wa nchi yoyote, lakini wengi wamekuwa wakiikosa haki hii kutokana na uwekezaji duni. Uwekezaji mdogo katika elimu unapunguza uwezo wa serikali kutoa elimu bora na iliyo sawa kwa wote. Nchini Tanzania, tunalazimika kusema kuwa, vikwazo vingi kwenye sekta ya elimu ni matokeo ya serikali kushindwa kuwekeza vya kutosha kwenye elimu.

Elimu nchini Tanzania imeandamwa na dhana au fikra ya "urithishaji wa hadhi ya elimu" tatizo la kidunia ambapo mafanikio ya watu ki-elimu kwa kiasi kikubwa hutegemea hali yao ya kiuchumi na hali ya elimu ya wazazi wao[1]. Hali hii hutokea katika mazingira ambapo serikali imeachia sekta binafsi kutoa elimu na hivyo kutokuwekeza vya kutosha katika sekta hiyo.

Kuondoa mtazamo huo, nchi inahitaji kuliweka jukumu la utoaji wa elimu chini ya serikali kuu na kulifanya kuwa jukumu lake la msingi. Mgao wa bajeti ndani ya sekta unapaswa kuwa mkubwa na unaoendana na mahitaji. Kwa hiyo, uchambuzi huu, unachunguza juhudi za serikali ya Tanzania kuelekea kuboresha bajeti ya elimu na uwekezaji kwenye elimu.

Je, serikali ya Tanzania inawekeza vya kutosha kwenye elimu? Je, hatua zinazochukuliwa zinatosha kushughulikia changamoto kwa ufanisi? Ni maeneo gani yana tija zaidi kuwekeza kwenye elimu? Kazi hii inajaribu kujibu maswali haya kwa kuchunguza ugharimiaji wa sekta ya elimu kwa mwaka 2014/15 na mwenendo wa matumizi ya siku za nyuma. Mwisho wa uchunguzi huu, msimamo wetu unapaswa kuamua; kwa upande mmoja, kama uwekezaji katika elimu ni muhimu na, kwa upande mwingine, kama ufinyu wa bajeti unazuia ugawaji rasilimali zilizopo, basi uwekezaji unapaswa kufanyika kikamilifu kadri iwezekanavyo.

## Changamoto za Sekta ya Elimu mwaka 2014/2015

Kabla ya kuzama kwenye tarakimu za bajeti na takwimu kama njia ya kupima ufanisi wa uwekezaji wetu katika elimu, hebu kwanza tuangalie changamoto zilizotazamiwa[2] kuwa vikwazo kwenye utoaji elimu iliyo bora na yenye usawa kwa mwaka wa fedha 2014/15. Hizi zilikuwa pia changamoto za msingi ambazo tulitarajia bajeti ya sekta ya elimu ya mwaka 2014/15 izishughulikie.[3]

Kabla ya vikao vya Bunge la bajeti kuanza mwezi Aprili 2014, HakiElimu ilifanya utafiti mfupi juu ya changamoto zinazoathiri ujifunzaji nchini Tanzania, na ambazo zilipaswa kushughulikiwa katika bajeti ya sekta ya elimu ya mwaka 2014/2015. Changamoto hizi zilikusanywa katika mfumo wa Tamko la Kabla ya Bajeti. Ujumbe wa Tamko hilo ulisambazwa kwa wabunge, wajumbe wa Kamati ya Bunge Huduma za Jamii na pia ulichapishwa kwenye magazeti ya ndani ya nchi na kwenye mitandao ya kijamii. Changamoto hizo ni pamoja na;

- Kuongezeka kwa malalamiko ya walimu
- Kuchelewa na kutolewa kiasi pungufu cha ruzuku ya uendeshaji shuleni
- Ukosefu wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya elimu ya awali
- Kukosekana kwa bajeti kwa ajili ya Idara ya Ukaguzi wa Shule
- Kutokuwepo kwa uwazi na uwajibikaji kwenye bajeti ya elimu
- Uwekezaji duni kwenye elimu

---

1 Tom Hertz, *at el* (2007) "Urithi wa Elimu isiyo na Usawa: Ulinganishi Kimataifa. Mwenendo wa Miaka hamsini," *The B.E. Jarida la Uchambuzi wa Kiuchumi & Sera*: Vol. 7: Iss. 2 (Advances), ( http://www.bepress.com/bejeap/vol7/iss2/art10)

2 Hotuba ya bajeti mbadala ya mwaka 2014/15 iliyotolewa na Waziri kivuli wa elimu Mhe. Susan Lyimo

3 Tamko la HakiElimu la Kabla ya Bajeti 2014 lililochapishwa kwenye magazeti ya mwananchi na Tanzania Daima

Kwa mujibu wa tamko la kabla ya bajeti, changamoto hizi zilipaswa kujadiliwa bungeni na kuzingatiwa wakati Serikali na Bunge wanapanga kugawa na kuidhinisha rasilimali katika bajeti ya elimu ya mwaka wa fedha 2014/2015. Kwa maoni ya HakiElimu, changamoto hizi zingeweza kushughulikiwa tu kwa kufanya "uchaguzi wenye tija kuwekeza kwenye elimu" na uchaguzi huo ulipaswa kuzingatiwa kwenye mgao wa bajeti ya elimu ya mwaka wa fedha 2014/15.

Kujua kama kweli serikali imewekeza vya kutosha kushughulikia changamoto hizi katika bajeti ya elimu ya mwaka 2014/15, kunaweza kuamriwa kwa kupitia na kufanya uchambuzi wa kina wa bajeti. Hiki ndiyo kiini cha ripoti hii; ambayo inafuatilia mwenendo wa ugharimiaji wa elimu, kuchambua bajeti na mgao wa elimu mwaka 2014/15 ili kufahamu kama Serikali imewekeza vya kutosha kukabiliana na changamoto zinazoongezeka.

## Muundo wa Bajeti ya Sekta ya Elimu kwa mwaka 2014/2015

Utoaji wa elimu nchini Tanzania siyo wajibu wa Wizara moja maalum: bali unafanywa na serikali kupitia Wizara kadhaa na idara mbalimbali. Wizara hizi ni; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (MoEVT); Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto (MCDWC); Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(OWM -TAMISEMI) na Tume ya Huduma za Umma. Vile vile bajeti ya sekta hutengwa na kutekelezwa na Wizara na idara hizi.

Jumla ya Mgao wa serikali kwa sekta nzima ya elimu mwaka 2014/2015 ni Sh bilioni 3,465 ambapo bilioni 2,656 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na bilioni 809 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kwa mujibu wa uchambuzi wa ki-sekta wa Wizara ya Fedha, kiasi cha Sh bilioni 799 tu, kati ya Jumla ya Bajeti nzima(bilioni 3,465) ndiyo kilipelekwa Wizara ya Elimu (Kasma na 46), bilioni 12 zilipelekwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii (Kasma 53), bilioni 13 zilipelekwa Tume ya Utumishi wa Umma (Kasma 94) na kiasi kilichosalia (takriban bilioni 2,638) hupelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI (Kasma 56).

Kwa hiyo, sehemu kubwa ya bajeti ya elimu (76%) huenda Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI ambayo ina wajibu wa kuratibu elimu-msingi (elimu ya msingi na sekondari), kurekebisha mishahara ya walimu na maafisa wa elimu na kuratibu shughuli na miradi ya serikali za mitaa na miradi ya mikoa. Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ina wajibu wa kutekeleza miradi mingi ya sekta ya elimu kupitia serikali za mitaa, wakati Wizara ya Elimu ina wajibu wa kutunga na kutekeleza sera pamoja na kutoa maelekezo na maagizo ya kiutendaji.

Tunaweza kujua kama Sh bilioni 3,465 ni uwekezaji wenye tija au la kwa kuangalia aina ya mgao wa bajeti yenyewe[4]. Aina ya mgawanyo inapaswa kutuambia kama kiasi na aina ya mgao vitafanikiwa kushughulikia changamoto zilizobainishwa kuwa  zinaathiri ufundishaji na ujifunzaji nchini kwetu.

Kama ilivyoelezwa hapo juu; kiasi cha Sh bilioni 2,656 kati ya bajeti nzima ya bilioni 3,465 (76%) kilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha bilioni 809 tu (24%) cha bajeti yote ya elimu ndiyo kilitengwa kwa matumizi ya maendeleo. Wataalam wa bajeti wanauona mgao huu wa matumizi kama uwekezaji mbaya, kwa tafsiri kwamba, kiasi kikubwa cha fedha kinapaswa kwenda kwenye matumizi ya maendeleo kuliko kwenye matumizi mengine. Ili uwekezaji uonekane makini na wenye ufanisi, matumizi ya maendeleo yanapaswa kuwa sawa au yawe zaidi ya matumizi ya kiutawala.

4 Mgao wa thamani ghafi dhidi ya thamani halisi, na uwiano kati ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo/ uwekezaji ya sekta.

**Kielelezo cha 1: Uwiano wa matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo sekta ya elimu kwa mwaka wa fedha 2014/2015**




Thamani ghafi ya fedha za sekta ya elimu inaonekana kuongezeka kwa 10% kutoka Sh bilioni 3,128 zilizotengwa mwaka 2013/2014 hadi kufikia Sh bilioni 3,465 mwaka wa fedha 2014/15, ongezeko la Sh bilioni 337. Hii inaweza kuonekana kuwa serikali imeongeza uwezo wake wa kutumia fedha kwenye elimu kwa 10% kwa mwaka 2014/15 ikilinganishwa na uwezo wake mwaka uliopita 2013/14.

Hata hivyo, ili kujua kama 10% ni ongezeko kubwa inategemea thamani halisi ya bajeti baada ya kuangalia mfumuko wa bei. Kiwango cha mfumuko wa bei ni muhimu kwa sababu kinaamua uwezo wa fedha kufanya manunuzi ya bidhaa na mahitaji wakati fulani. Na kwa sababu kiwango cha mfumuko wa bei kimekuwa kikipanda[5] ongezeko la 10% halipaswi kuchukuliwa kama ongezeko kubwa la bajeti, bali ni kitu cha kawaida tu katika "marekebisho ya mfumuko wa bei".

Hata hivyo, kama tukikokotoa kiwango cha mfumuko wa bei kwa kuangalia Faharasa ya Bei za Walaji (CPI) kwenye elimu, ambayo ilikuwa 140 mwezi Juni 2013 na 149 mwezi Julai 2014, Tunaweza kusema mgao halisi wa bajeti (uwezo wa kununua) kwa mwaka 2014/15 utakuwa kiasi cha Sh bilioni 3,255 kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini ikionesha ongezeko bajeti ghafi ya sekta na bajeti halisi ya sekta:-

**Kielelezo cha 2: Ongezeko ghafi katika bajeti ya sekta ya elimu 2014/2015**




5 http://sw.tradingeconomics.com/Kiwango cha kushuka kwa thamani ya fedha Tanzania kiliongezeka hadi kufikia asilimia 6.5 mwezi Mei mwka 2014, kutoka asilimia 5.6 mwezi Januari mwaka huuhuu, hii ilichangiwa na ongezeko la bei za vyakula. Hiki ni kiwango cha juu kushuhudiwa tangu mwezi Septemba 2013. (Ilichapishwa tarehe 09-06-2014)

**Kielelezo cha 3: Ongezeko halisi katika bajeti ya sekta ya elimu mwaka wa fedha 2014/2015**




Hii inamaanisha uwezo wa bajeti ya elimu ya mwaka 2014/15 kununua au kutekeleza mipango na shughuli ni Sh bilioni 3,255 badala ya bilioni 3,465 ambazo zinaonekana kwenye mgao wa jumla(ghafi).

Hivyo, kama thamani halisi ya bajeti ya mwaka 2014/15 sh bilioni 3,255 ikilinganishwa na Sh bilioni 3,128 za bajeti ya mwaka 2013/14 kama ilivyooneshwa katika kielelezo cha 3 hapo juu, tofauti ya thamani baina ya bajeti hizi mbili inakuwa ni Sh milioni 127 tu. Hii inatusukuma kujiuliza iwapo Sh milioni 127 ni ongezeko kubwa kiasi cha kutosha? Je, kwa ongezeko hili, tunaweza kusema huu ni uwekezaji makini kwenye elimu?

## Bajeti ya Elimu ikilinganishwa na Bajeti ya Taifa

Njia mojawapo ya kuelewa iwapo serikali iko makini kuwekeza kwenye elimu ni kuangalia uwiano kati ya bajeti za sekta dhidi ya bajeti ya taifa. Kwa mujibu wa hotuba ya bajeti ya taifa ya mwaka 2014/15, Bajeti nzima ya Tanzania kwa mwaka wa fedha 2014/15 ni Sh bilioni 19,853. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 1,604 kutoka kiasi cha Sh bilioni 18,249 za bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014. Hata hivyo, kama tulivyoona hapo juu, bajeti ya sekta ya elimu iliyotengwa kwa mwaka 2014/15 ni Sh bilioni 3,465.

Kwa kukokotoa, Sh bilioni 3,465 ni karibu 17% ya jumla ya bajeti ya taifa (ambayo ni Sh. bilioni 19,853). Lakini swali linabakia kuwa, Je ni kweli kuwa 17% ya bajeti ya taifa ni mgao wa kutosha kwenye sekta ya elimu? Kwa kuzingatia kuwa siyo fedha zote zilizotengwa (bilioni 3,465) huenda kwenye miradi ya uwekezaji na badala yake ni shilingi bilioni 809 tu ambayo ni 24% ya bajeti yote ya sekta ya elimu ndiyo imetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kiasi kilichobaki, takriban Sh bilioni 2,656 ambayo ni sawa na 76% ya mgao wa sekta ya elimu inatumika kugharimia matumizi ya kawaida (yaani mishahara, posho, mikutano, ukarimu nk) kama tulivyoona pale mwanzo.

Mantiki yake ni rahisi, upatikanaji wa elimu bora na yenye usawa unategemea zaidi uwekezaji katika vifaa na vitendeakazi kama miundombinu, vitabu, maktaba, maabara na mazingira rafiki ya kujifunzia. Lakini kama tulivyoona, ni 24% tu ya fedha za bajeti ya elimu ndizo zimeelekezwa kwenye maeneo muhimu, wakati 76% zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kutenga fedha nyingi zaidi kwenye matumizi ya kawaida kuliko matumizi ya maendeleo kuna maanisha kushughulikia changamoto chache zaidi. Na ukweli ni kuwa, utatuzi wa matatizo makubwa katika elimu nchini Tanzania unahitaji mgao mkubwa zaidi kwenye miradi ya maendeleo kuliko matumizi ya kawaida[6].

Ingawa ikilinganishwa na sekta nyingine, bilioni 3,465.1 zilizotengwa kwa ajili ya sekta ya elimu zinaifanya sekta ya elimu kushika nafasi ya kwanza katika mpangilio wa vipaumbele; ikifuatiwa na uchukuzi na miundombinu ambavyo vina Sh bilioni 2,109 kama ilivyooneshwa kwenye tarakimu za mgao wa kisekta hapa chini; -

6 Rejea hotuba ya bajeti mbadala iliyotolewa Waziri kivuli wa elimu

**Kielelezo cha 4: Mgao kisekta kwa mwaka wa fedha 2014/2015**




Hivyo, tunaweza kusema kuwa jambo zuri kuhusu mgao wa bajeti ya elimu kwa mwaka 2014/15 ni kwamba, sekta ya elimu imepewa kipaumbele cha kwanza kwenye mgao wa fedha. Angalau hii inaonesha dhamira ya serikali, na kwa hili serikali inapaswa kupongezwa. Tunaiomba serikali iendelee kuiweka elimu kuwa kipaumbele cha kwanza siyo tu katika mgao wa fedha lakini pia katika upelekaji fedha na usimamizi wa utendaji.

Ingawa Mkataba wa Elimu kwa Wote (EFA-2000) kupitia mwongozo wa kiutendaji wa Dakar haukutaja kiasi gani nchi zinapaswa kutenga kwa ajili ya elimu, shabaha ya ugharamiaji wa malengo ya EFA baada ya mwaka 2015 iko bayana kuwa nchi zinapaswa kutenga fedha kwa ajili ya elimu angalau 6% ya Pato la Taifa, au kama inavyokubaliwa sehemu nyingi duniani, nchi zinapaswa kutenga angalau 20% ya bajeti zao za kitaifa kwa ajili ya sekta ya elimu[7].

Kwa hiyo, kwa mujibu wa malengo ya EFA na utaratibu uliokubaliwa kimataifa, Tanzania haiwekezi vya kutosha kwenye elimu. Hii siyo tu kukiuka malengo ya EFA ambayo Tanzania ilisaini lakini pia hailingani na changamoto zinazojitokeza ambazo zinakwamisha ujifunzaji nchini; jambo ambalo limeathiri sana utoaji wa elimu nchini Tanzania kwa miaka mingi.

Hata hivyo, ilikuwa mwaka 2008/2009 tu ambapo serikali iliweza kutenga 20% ya bajeti yake ya taifa kwenye sekta ya elimu. Tangu wakati huo kiasi kimekuwa kikipungua kila mwaka. Kielelezo hapo chini kinaonyesha hili; -

7 Ripoti ya Kimataifa ya ufuatiliaji wa EFA ya 2013/14; Ufundishaji na Ujifunzaji Kufikia Elimu bora kwa wote; uk 23: Kati ya nchi 138 zenye takwimu, ni nchi 25 tu hutumia 20% ya bajeti kwenye elimu mwaka 2011. Tanzania inatumia 17% tu.

**Kielelezo cha 5: Bajeti ya sekta ya elimu kwa uwiano na bajeti ya Taifa**




Hili ni jambo linalosumbua kabisa na linaibua maswali mengi juu ya dhamira na nia ya dhati ya serikali kuweka kipaumbele kwenye elimu. Hii ni kwa sababu ingawa bajeti ya taifa imekuwa ikiongezeka kila mwaka kwa uwiano wa bajeti ya elimu kama sehemu ya bajeti ya taifa umekuwa ukipungua.

**Kielelezo cha 6: Mwenendo wa mgao wa bajeti ya taifa**




## Bajeti ya Wizara ya Elimu

Vitabu vya makisio na kiasi cha fedha za bajeti kilichopitishwa vinaonesha kuwa bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeongezeka kutoka Sh. Bilioni 689.7 mwaka 2013/2014 hadi Sh. Bilioni 794 mwaka 2014/2015. Hili ni ongezeko la Sh bilioni 104 (15.1%) zaidi ikilinganishwa na bajeti ya Wizara ya mwaka 2013/14. Kiasi cha bilioni 454 kati ya bajeti nzima ya Sh bilioni 794 zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo na bilioni 340 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hii ina maana kuwa mgao wa fedha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo umeongezeka kutoka Sh bilioni 72 zilizotengwa mwaka jana hadi kufikia sh bilioni 454 mwaka huu, wakati ambapo mgao wa matumizi ya kawaida umeshuka kutoka sh bilioni 612 zilizotengwa mwaka jana hadi Sh bilioni 340 mwaka huu 2014/15.

**Kielelezo cha 7: Mgao wa bajeti sekta ya Elimu**




Grafu hapo juu inaonesha mgao wa bajeti ya wizara ya elimu mwaka 2014/15 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ikipanda hadi 57% ya bajeti ya nzima ya wizara, wakati mgao kwa ajili ya matumizi ya kawaida umeshuka hadi 43% ya bajeti nzima ya wizara. Hiki ni kiashiria kizuri cha uwiano kati ya bajeti ya maendeleo na bajeti ya matumizi ya kawaida ambayo imepunguzwa hadi kufikia Sh bilioni 340 mwaka huu kutoka Sh bilioni 612 zilizotengwa mwaka jana. Kwa mwaka 2013/14, bajeti ya matumizi ya maendeleo ilikuwa 10% tu ya bajeti nzima ya Wizara, wakati 90% ya bajeti nzima ya wizara ilipelekwa kwenye matumizi ya kawaida.

**Kielelezo cha 8: Matumizi ya kawaida vs. Matumizi ya maendeleo ya Wizara**




Hata hivyo, tahadhari inahitajika kabla ya kupongeza tarakimu hizi zilizopitishwa. Ingawa kuna ongezeko katika tarakimu, lakini kiuhalisia bajeti ya Wizara ya matumizi ya maendeleo imepunguzwa. Ongezeko linaloonekana ni la matokeo ya kiutaratibu na siyo ongezeko halisi. Ni matokeo ya kuhamisha kifungu namba 7001 kutoka Mgao wa Elimu ya Juu ambacho mwaka 2013/14 kilichukuliwa kama fedha za matumizi ya kawaida, ambacho kwa sasa kimeondolewa na kupelekwa kwenye kifungu kidogo namba 1003 cha (Sera na Mipango, ambayo ni matumizi ya Maendeleo) kwa mwaka 2014/15.

Kulingana na vitabu vya makadirio ya bajeti, jumla ya Sh bilioni 306 kati ya Sh bilioni 454 zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo zinakwenda Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kama mikopo ya wanafunzi. Kiasi hiki ni 68% ya bajeti ya matumizi ya maendeleo ya Wizara ya Elimu. Kwa hiyo, kiuhalisia ni 33% tu ya bajeti nzima ya matumizi ya maendeleo ya Wizara (Sh bilioni 148.) ndiyo inabaki kwa ajili ya utekelezaji wa miradi halisi ya maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2014/15.

**Kielelezo cha 9: Uwiano wa bajeti ya wizara ya matumizi ya maendeleo**




Kwahiyo tafsiri ya hapa ni kwamba, sehemu kubwa ambayo inatajwa kama matumizi ya maendeleo haiendi kwenye matumizi halisi ya maendeleo, lakini badala yake inakwenda Elimu ya Juu kama mikopo ya wanafunzi kwa matumizi yao ya kawaida. Iwapo mikopo ya wanafunzi 'inapaswa kuchukuliwa kama uwekezaji au la, ni jambo linalohitaji mjadala na hii ni kwa sababu mikopo hii haina riba na ulipaji wake umekuwa hauna ufanisi.

Hivyo, kwa sura hii ya bajeti ya wizara, ni wazi kuwa Wizara bado inatumia kiasi kidogo kwenye miradi ya elimu zaidi ya inavyotakiwa na bado inatumia kiasi kikubwa kwenye matumizi ya kawaida isivyopaswa. Je, huu ni uwekezaji wenye tija? Jibu la swali tunaomba kuliacha wasomaji na umma kwa ujumla. Hivyo, soma na jibu lako litahesabiwa kama moja ya ushauri kwa serikali.

## Uwekezaji kwenye Elimu ya Awali

Kwa ujumla, Watafiti wanakubaliana kuwa kuwekeza katika elimu ya makuzi na malezi ya utotoni ina manufaa makubwa baadaye. Mshindi wa Tuzo ya Nobel[8] aliwahi kusema "uwekezaji wa mapema unaongeza fursa sawa na kuleta mafanikio makubwa; wale wanaotaka kupunguza umaskini na kuimarisha uchumi wanapaswa kuwekeza vya kutosha kwenye elimu ya makuzi na malezi ya utotoni". Swali ni hili; kama nchi tunawekeza vya kutosha katika elimu ya makuzi na malezi ya utotoni?

Ingawa umuhimu wa kuwekeza kwenye elimu ya makuzi na malezi ya utotoni umeoneshwa kupitia sera na mipango mbalimbali nchini Tanzania[9], serikali imeshindwa kuweka matamanio hayo kwenye uwekezaji halisi. Mathalani, uchambuzi wa makisio ya bajeti ya mwaka 2014/2015, bajeti iliyopitishwa na bunge, katika hotuba ya bajeti ya wizara husika na sekta yenyewe unaonesha kuwa hakuna fedha ambayo imewahi kutengwa mahsusi kwa ajili ya elimu ya Awali.

MMEM III unaitaka serikali kuinua ubora wa elimu ya awali kwa kutoa ruzuku ya Sh 10,000 kwa kila mwanafunzi wa darasa la awali kwa mwaka na shilingi 20,000 kwa kila mwanafunzi mwenye mahitaji maalum. Hata hivyo, hadi sasa hakuna, ushahidi wowote wa utolewaji wa fedha hizo kutoka Hazina wala hakuna ushahidi wa kupokelewa shuleni, ikiwa ni fedha mahsusi kwa ajili ya kusaidia kuboresha elimu ya awali.[10]

Makisio ya fedha za MMEM yanaonesha[11] kuwa serikali inatakiwa kujenga madarasa ya awali 106,158 ili kuondoa mlundikano wa watoto madarasani na kwenye vituo vya elimu ya awali ifikapo mwaka 2016. Hii ina maana kwamba madarasa 60,606 lazima yajengwe mwaka 2014/15 na kuajiri walimu wa madarasa ya awali 68,391 ili kufikia ikama ya uwiano wa 1:25 ifikapo mwaka 2016. Aidha, zaidi ya walimu 7,300 lazima waajiriwe mwaka 2014/15 ili kupandisha uwiano wa sasa wa 1: 124.

8 Prof. James J. Hackman Chuo Kikuu cha Chicago; Makala; Kuwekeza kwenye Makuzi na Malezi ya Awali ya mtoto; Kunapunguza Mapungufu, na Kuimarisha Uchumi

9 Sera ya Elimu na Mafunzo (ETP) ya 1995, Mtaala wa Elimu ya Awali, 2007, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) I – III n.k

10 (angalia rejeo na 8 hapo chini)

11 (Uchambuzi wa mahitaji na Makisio ya Fedha ya MMEM III.)

Aidha, makisio yanaonesha hitaji la kukarabati na kuweka samani madarasa ya awali yapatayo 4201 ifikapo mwaka 2016; ujenzi wa viwanja vya michezo 3,000 na matundu ya vyoo 63,119 kwa ajili ya madarasa ya awali ifikapo mwaka 2016. Pia Makisio yanaonesha kuwa jumla ya viti na meza 127,381 vinapaswa kununuliwa kwa ajili ya walimu awali na msingi ifikapo mwaka 2016, na jumla ya madawati 336,162 yanapaswa kununuliwa kwa ajili ya walimu wa awali ifikapo mwaka 2016.

Hata hivyo, makadirio hayo yametokana na mawazo kwamba, serikali imedhamiria kutoa ruzuku ya uendeshaji ya Sh 10,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka[12]; na kwamba wastani wa kiwango cha mfumuko wa bei utabaki kwenye tarakimu moja kwa kipindi cha utekelezaji wa MMEM III; na kwamba mapato ya ndani yataongezeka kwa 19% ya Pato la Taifa ifikapo 2015/16. Aidha, taifa lilikadiria kufikia ukuaji wa Pato la Taifa wa 8.5% ifikapo mwaka 2015 *(Miongozo ya Bajeti - 2012/13-2015/16*) na ingeweka ahadi ya kutenga hadi 20% ya jumla ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya Sekta ya Elimu.

Hii ina maana kwamba uchaguzi wa serikali kuwekeza kwenye elimu ya awali ni kitu cha kufikirika tu. Ingawa masharti kama vile kutenga 20% ya matumizi ya kawaida ya taifa kwenda kwenye elimu yametimizwa, masharti ya msingi sana kama kutoa Sh 10,000 kama ruzuku ya uendeshaji, kuongeza pato la ndani kwa 19% ya Pato la Taifa na kulinda mfumuko wa bei kwenye tarakimu moja vimebaki kuwa ndoto. Je, makadirio yatafikiwa bila fedha zinazotakiwa? Je, serikali inaelewa kivitendo thamani ya elimu ya makuzi na malezi ya awali na uhusiano wake na ukuaji wa uchumi na kijamii? Maswali haya yanahitaji majibu ya kiutendaji; siyo tu suala la kuelezea kwenye sera na mipango: yanapaswa kutafsiriwa kwenye mgao halisi wa fedha na kwenye utoaji pia.

Serikali inapaswa kutimiza ahadi ilizotoa kwenye MMEM III; kuzitafsiri ahadi za kutenga 20% ya fedha kwa ajili ya sekta ya elimu, na angalau 60% ya bajeti ya sekta kwenye elimu ya awali na msingi. Bila kufanya hivyo, hatuwezi kudai kwa uhakika kuwa tunafanya uwekezaji wa kutosha kwenye elimu ya makuzi na malezi ya utotoni.

## Hadaa katika utoaji ruzuku ya uendeshaji

Ili kuboresha upatikanaji, usawa, ubora, uwezo kiutawala na usimamizi wa elimu; Serikali ya Tanzania ilianzisha programu mbili kubwa mwanzoni mwa miaka ya 2000. Programu hizo ni Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) mwaka 2002, uliolenga kufanikisha utoaji Elimu kwa Wote (UPE) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) mwaka 2004.

Ili kufikia malengo haya, serikali iliahidi kuziwezesha kifedha shule za umma ili zijiendeshe zenyewe ili kutoa elimu bora. Uwezeshwaji huu ulikuwa katika mfumo wa utoaji ruzuku ya uendeshaji kwa kila shule kulingana na idadi ya wanafunzi. Ahadi ilikuwa ni kutoa Sh. 10,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kwa shule za msingi, na Sh 25,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kwa shule za sekondari. Ruzuku hii ilipaswa kutumika katika kununulia vitabu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ujenzi na ukarabati na kusaidia shughuli za utawala na usimamizi wa shule.

Ingawa kumekuwa na matokeo chanya yatokanayo na utekelezaji wa mipango hii, matahalani kuongeza kwa Uandikishaji wa Jumla (GER), na Uandikishaji Halisi (NER)[13] na ongezeko la idadi ya shule za msingi na sekondari, ripoti[14] zinaonesha kuwa mgao wa ruzuku kwa kila mwanafunzi unakabiliwa na changamoto lukuki hasa kutokana na kiasi cha fedha zinazotengwa mara nyingi huwa chini zaidi kuliko bajeti iliyopangwa, na fedha kuchelewa kuwasilishwa shuleni.

Matokeo ya kuwepo kwa changamoto hizi kumekwamisha kufikia shabaha na malengo yaliyopangwa kwenye program zote mbili za MMEM na MMES awamu ya I na II. Changamoto hizo ziliathiri vibaya mafanikio ya malengo yaliyowekwa. Matokeo yake ukarabati wa madarasa yaliyopo na ujenzi wa madarasa mapya, kwa mfano, haukuweza kufikia lengo la uwiano wa darasa kwa mwanafunzi (CPR) la 1:40 kutoka kwenye uwiano wa sasa wa 1:66 (2013). Upungufu wa madawati ni takriban 49.1% ya mahitaji.

12 Kujua kama serikali itatimiza ahadi hii au la, kutajadiliwa kikamilifu kwenye mada inayofuata; Kuwekeza kwenye Ruzuku ya Uendeshaji"

13 GER–Uwiano wa Uandikishaji wa jumla; NER– Uandikishaji Halisi

14 Ripoti za utekelezaji wa MMEM na MMES

Kwa mujibu wa ripoti za utekelezaji wa MMEM II na MMES I, utekelezaji wa mipango hii ulikuwa wa takriban 55% pekee. Shule zilipokea wastani wa Sh 5,500 kama ruzuku kwa shule za msingi badala ya Sh 10,000 iliyopangwa na ruzuku ya wanafunzi wa shule za sekondari Sh. 13,500 badala ya 25,000 iliyopangwa. Hii ina maana kuwa karibu 46% ya malengo ya kupeleka ruzuku shuleni hayakufikiwa. Jedwali hapa chini linafafanua suala hili.

**Jedwali la 1: Hali ya utoaji na upelekaji wa ruzuku ya uendeshaji**

| | Iliyopangwa | Iliyopokelewa | Mapungufu | Uwiano wa mapungufu |
|---|---|---|---|---|
| MMEM II | 10,000 | 5,500 | 4,500 | 45% |
| MMES I | 25,000 | 13,500 | 11,500 | 46% |

Lakini, hata baada ya kujifunza kutokana na uzoefu wa zamani na kuanzishwa kwa MMEM III na MMES II, utoaji wa ruzuku kwa ukamilifu na kwa wakati bado ni changamoto kubwa.

Kwa mfano, kwa mujibu wa utafiti[15] uliofanywa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14; wastani wa kiasi cha fedha-kwa kila mwanafunzi kilichopokelewa kwenye shule zilizofanyiwa utafiti (shule za msingi) kilikuwa Sh. 2700 badala ya Sh. 10,000. Na Sh. 11,462 kwa kila mwanafunzi (shule za sekondari) badala ya Sh 25,000 iliyotarajiwa.

**Kielelezo cha 10: Wastani wa ruzuku kwa robo mwaka msingi**




**Kielelezo cha 11: Wastani wa ruzuku kwa mwaka msingi**




**Kielelezo 12: Wastani wa ruzuku kwa robo za mwaka sekondari**




**Kielelezo 13: Wastani wa ruzuku kwa mwaka sekondari**




15 HakiElimu 2013/14 Ufuatiliaji wa Matumizi ya fedha za Umma juu ya Ruzuku ya Uendeshaji

Ingawa kuna hoja kuwa upungufu huu wakati mwingine husababishwa na ununuzi wa moja kwa moja wa vitabu chini ya utaratibu wa "Chenji ya Radar"[16] ambapo 40% ya ruzuku pia hutumika, ukweli ni kwamba upungufu huu umekuwepo muda mrefu tangu kuanzishwa kwa MMEM na MMES mapema miaka ya 2000 kabla hata "Chenji ya Radar" haijajulikana. Hii inaonesha kuwa serikali haijawa makini kiasi cha kutosha katika ugawaji na upelekaji rasilimali hizi za ruzuku shuleni!

## Utegemezi katika ugharamiaji wa sekta ya elimu

Fedha ambazo hugharimia sekta ya elimu nchini Tanzania zinatoka vyanzo vikuu vinne; mapato ya ndani ya Serikali, Mfuko wa pamoja wa misaada ya wahisani; Misaada ya miradi na; wadau wengine ikiwa ni pamoja na wazazi, mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi. Kwa bahati mbaya, serikali ina taarifa juu ya vyanzo vitatu vya kwanza vya fedha. Lakini michango ya wadau wengine, ambayo pia ni mikubwa na muhimu, haizingatiwi vya kutosha[17].

Fedha za Mfuko wa pamoja wa Msaada wa bajeti, hupelekwa moja kwa moja Serikalini kutoka serikali za wahisani au Mashirika ya kimataifa ya misaada ya maendeleo kama Shirika la Fedha Duniani (IMF) kupitia Wizara ya Fedha kwa ajili ya matumizi ya umma. Kwa upande mwingine, Misaada ya kuchangia miradi ni fedha za misaada ya maendeleo zinazotumiwa na wafadhili kutekeleza miradi maalum, na wafadhili wanachukua jukumu la kudhibiti matumizi ya fedha na usimamizi wa mradi.

Utegemezi wa Bajeti umekuwa utamaduni wetu nchini Tanzania; kwa mfano, mwaka 2012/2013 matumizi halisi ya maendeleo ya Wizara yalikuwa ni shilingi bilioni 59.5 ambapo shillingi bilioni 8.4 (14%) zilitoka vyanzo vya ndani na bilioni 51.1(86%) zilikuwa fedha kutoka nje (utegemezi wa wafadhili). Mwaka 2013/2014 bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Elimu ilikuwa Sh bilioni 72.5; kati ya hizo bilioni 18.8 (26%) zilitoka vyanzo vya ndani na bilioni 53.7 (74%) ilitoka kwa wafadhili.

**Kielelezo cha 14: Utegemezi katika sekta ya Elimu**




Hata kwenye miradi maalum, Serikali inategemea wafadhili. Kwa mfano, kwenye bajeti ya elimu ya mwaka 2014/2015, serikali imetenga takriban shilingi bilioni 203.2 kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Elimu ya msingi na sekondari (MMEM III & MMES II), lakini Sh bilioni 93.6 (46%) ya jumla ya fedha zote zinatarajiwa kutoka kwa wafadhili na shilingi bilioni 109.6 tu ambazo ni (54%) ya jumla ya fedha zote ndiyo zitakusanywa kutoka mapato ya ndani.

Utegemezi katika bajeti umekuwa kikwazo kikubwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha za wafadhili kwa kawaida huja na masharti magumu, na wakati mwingine wafadhili hushindwa kutoa fedha kama walivyoahidi. Kwa mfano, mwaka 2013/2014, Wizara ilitumia Sh bilioni 14 (19%) tu ya bajeti nzima

16 Kiasi kilichorudishwa Tanzania na serikali ya Uingereza baada ya kushutumiwa kuwa Ununuzi wa Radar ya dola milioni 44 (Sh bilioni 70) kutoka Kampuni ya Uingereza ya British Aerospace Engineering (BAE Systems) uligubikwa na rushwa. Iliamriwa kuwa fedha iliyorudishwa itumike kununulia vitabu.

17 Michango ya Kaya kwenye ugharamiaji wa elimu inakadiriwa kuwa sawa na 32.1% matumizi ya elimu ya umma kwa mujibu wa shirika la elimu duniani UNESCO.

ya maendeleo ya bilioni 72. Kwa mujibu wa Waziri wa Elimu[18] utoaji wa fedha usio wa uhakika kutoka kwa wafadhili ilikuwa ni sababu mojawapo ya kutumia fedha chini ya kiasi kilichotengwa. Wafadhili waliahidi kuchangia kwenye bajeti hiyo bilioni 53.7, lakini walitoa bilioni 8.3 tu, ambayo ni 15% ya kiasi walichoahidi.

Kama vile uzoefu wa mwaka jana haukuwa na maana, wizara imewataja tena wafadhili hao hao kuwa ndio watakaotoa fedha za bajeti kiasi cha bilioni 71.1 kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2014/15. Swali muhimu ni kuwa: kama wafadhili hao walishindwa kutoa bilioni 53.7 mwaka jana, nini kinaifanya serikali iamini kwamba wafadhiri haohao watatimiza ahadi yao safari hii?

Tafsiri ya kutegemea fedha za wafadhili ni kwamba, serikali itakuwa na uwezo wa kutekeleza miradi kama tu wafadhili watatoa fedha na kwa kiasi tarajiwa. Je, tunaweza sasa kusema kuwa tunawekeza kwa ufanisi kwenye elimu? Ni dhahiri HAPANA! Uwekezaji unakuwa na ufanisi tu kama fedha zinatolewa kwa uhakika, fedha za wahisani haziwezi kutegemewa kama tulivyothibitisha hapo juu.

## Hoja Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG) katika sekta ya elimu

Uwekezaji wenye ufanisi hauishii kwenye ugawaji makini wa rasilimali tu; bali huenda zaidi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali na utendaji. Kuamua kama serikali imekuwa ikiwekeza kikamilifu kwenye elimu, tunahitaji pia kuangalia aina ya matumizi na usimamizi wa fedha ndani ya sekta.

Katika taarifa ya ukaguzi wa hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2013; iliripotiwa kuwa fedha kwa ajili ya ruzuku ya uendeshaji shule kiasi cha Sh milioni 1,356 zilipokelewa kwenye Mamlaka 17 za Serikali za Mitaa lakini hazikupelekwa kwenye shule husika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo na uendeshaji. Hii ilisababisha kuchelewa kwa utoaji huduma zilizotarajiwa shuleni. Pia ilibainika kuwa, katika Halmashauri nne fedha za ruzuku kiasi cha Sh Milioni 498 zilitumika kugharimia matumizi ambayo hayahusiani na maeneo zilikopaswa kutumika ruzuku za wanafunzi, kwa mfano kulipa posho.

Iliripotiwa pia kwamba, katika kipindi cha mwaka uliomalizika, kulikuwa na fedha ambazo hazikutumiwa(bakaa) kiasi cha Sh. Milioni 1,138 kwenye halmshauri 13, fedha hizi zilitengwa kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Pia Sh Milioni 21,869 zilitolewa kwenda halmshauri kwa ajili ya kugharimia shughuli za MMES zinazolenga kuinua ubora, kupanua udahili wa wanafunzi sekondari na kuendelea kubaki shuleni kwa wanafunzi ngazi ya shule za sekondari. Hata hivyo, hadi mwisho wa mwaka Sh Milioni 11,207 (51%) tu ndizo zilikuwa zimetumika na kuacha kiasi Sh. 10,661 (49%) bila kutumika kwenye halmashauri 60.

Baadhi ya mapitio yalifanywa kuhusu usimamizi wa shughuli za Bunge zinazogharimiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwenye halmshauri 66, iligundulika kuwa halmshauri hizi zilibakiza fedha kiasi cha Sh Milioni 2,591. Fedha hizi zilipaswa kusaidia halmashauri kuchagiza maendeleo kwenye maeneo husika ikiwa ni pamoja na kuboresha elimu.

Mbali na usimamizi huu mbaya wa fedha ndani ya sekta ambayo imesababisha kushindwa kutumia fedha, ripoti ya ukaguzi pia iliripoti kuwa shule zote za msingi na sekondari zilikuwa na upungufu mkubwa wa walimu jambo ambalo limeathiri sana ubora wa elimu. Tatizo limesababisha nchi kushindwa kufikia lengo la uwiano wa kitaifa 1:45 (wanafunzi 45 kwa mwalimu mmoja). Mwelekeo unaonesha kuwa walimu wengi hawaripoti kwenye vituo vyao vya kazi hasa maeneo magumu kufikika vijijini.

Iwapo kiasi cha fedha ambazo hazikutumika ni kiasi cha Sh milioni 16,244 kama ilivyoripotiwa na CAG, kingetumika kujenga nyumba za walimu maeneo ya vijijini, jumla ya nyumba 464 zingejengwa. Hii ingepunguza uhaba wa nyumba za walimu na kuwatia moyo walimu kubaki kazini hasa maeneo ya vijijini yenye changamoto kubwa za miundombinu.

Inashangaza kuona sekta ambayo ina changamoto nyingi za fedha, inabakiza kiasi kikubwa cha fedha bila kutumika! Je, tunaweza kusema kwa dhati kuwa uwekezaji wetu kwenye elimu umekuwa wa ufanisi? Dhahiri kuwa ni HAPANA! Ni wazi kuwa elimu bora na yenye usawa haitafikiwa ikiwa usimamizi wetu wa fedha zinazotengwa ni mbovu namna hii. Serikali inapaswa kuelewa kwamba kutumia fedha chini ya kiwango na usimamizi mbaya wa fedha zinazotengwa ni kitu kibaya na ni uwekezaji mbaya pia.

18 Mhe. Shukuru Kawambwa-Waziri wa Elimu, akilihutubia Bunge mwaka 2014

**Kielelezo cha 15: Matokeo ya Ukaguzi juu ya hali ya matumizi ya fedha serikali kuu na serikali za mitaa yakionesha matumizi ya fedha sekta ya elimu, mapato yaliyopotea na uchambuzi kuonesha thamani yake.**




## Hitimisho & Mapendekezo

Ni wazi kabisa kuwa bado uwekezaji wa serikali kwenye sekta ya elimu unakabiliwa na changamoto kubwa. Ingawa tunapongeza juhudi zilizofanywa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kuipa kipaumbele sekta ya elimu kwa kutenga fedha nyingi zaidi; hatuwezi kusema uwekezaji huu umekuwa wenye tija. Ripoti hii ni ushahidi wa baadhi ya mapengo yanayohitaji kuzibwa.

Mtazamo mbadala wa uwekezaji kwenye elimu ni kuwa mgao wa fedha unapaswa kuwa mkubwa kwenye maeneo ambayo matatizo ni makubwa zaidi. Kwahiyo, ni muhimu uwekezaji ujao kwenye sekta ya elimu uzingatie changamoto halisi ambazo zinaathiri sana ujifunzaji na ubora wa elimu. Kama kuboresha upatikanaji elimu yenye usawa na thamani kunahitaji kuwekeza kwenye miundombinu, vitabu, maabara na motisha kwa walimu kama ilivyoelezwa kwenye uchambuzi wa mahitaji, inabidi, bajeti ya matumizi ya maendeleo katika maeneo haya iwe kubwa kuliko bajeti ya matumizi ya kawaida.

Programu maalum ya kusaidia elimu kwa makundi maskini ni muhimu, kwa maana zipo tofauti kwenye fursa ya kupata elimu kwa jinsia na maeneo wanayoishi, na hupungua kadri ngazi za elimu zinavyopanda juu. Hata hivyo, kigezo kikubwa cha ubaguzi kwenye elimu ni kipato cha familia, wale wanaotoka familia zenye kipato kizuri wana fursa pana ya kupata elimu bora na kufanikiwa maishani au kinyume chake.{Uwezo, 2010-2013}.

Wasichana, hususani wale wanaotoka katika familia maskini vijijini wanakabiliwa na mazingira duni ya upatikanaji wa elimu na mazingira duni ya kuwawezesha kubaki shuleni hadi watakapohitimu. Hii ina maana kuwa serikali inapaswa kuweka jitihada kubwa kukabiliana na mapungufu ya elimu na inapaswa kutenga fedha zaidi kwa ajili ya programu za watoto kutoka familia maskini ambao wako nyuma. Tafiti nyingi zinaonesha kuwa mapungufu kwenye elimu kimsingi ni tatizo kwa jamii nzima: hivyo, kila mtu atafaidika iwapo idadi ya watu wenye elimu ndogo na duni itapungua.. Kwahiyo, tunaweza kusema, elimu ina mchango mkubwa kwa maendeleo ya kijamii na binadamu, hasa kwenye ujuzi wa kusoma na kuandika, umaskini, uzazi, na kwenye afya ya uzazi na ya mtoto.

Mwisho, mgao wa fedha unapaswa pia kuendana na upelekaji fedha kama kweli serikali inamaanisha inachokisema kuhusu azma yake kufanikisha elimu kwa usawa na elimu bora kwa wote. Suala la kupungua kwa ruzuku ya uendeshaji na utoaji fedha wa wafadhili ni dalili mbaya kwetu, maana inaiweka sekta ya elimu kwenye hatari ya kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa kiwango kinachotakiwa.

Serikali inapaswa kuelewa kuwa uwekezaji halisi hauishii katika kugawa fedha; uwekezaji wa maana pia unahitaji usimamizi makini wa rasilimali na utekelezaji. Serikali inapaswa kutumia na kusikiliza ushauri na kutekeleza  mapendekezo yaliyomo katika ripoti za CAG juu ya mwenendo wa matumizi. Haingii akilini kusikia kila mwisho wa mwaka kuwa fedha zimebaki hazikutumika wakati sekta bado inakabiliwa na vikwazo vingi vya kifedha.

Kwa kuhitimisha, ingawa kutoa elimu kunabaki kuwa moja ya majukumu muhimu zaidi ya serikali yoyote ile, wananchi pia wana jukumu la kushawishi upatikanaji wa elimu bora kwa kila mtu. Kwa hiyo, wananchi wanahitaji kufuatilia mwenendo wa uwekezaji ndani ya sekta ili kuhakikisha kuwa kuna miundombinu mizuri ya elimu kwa ajili ya elimu isiyo na mwisho. Sekta binafsi pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali yanapaswa pia kutoa vifaa vya ziada badala ya kuiachia serikali kila kitu.

**Marejeo**


1. EFA Global Monitoring Report 2013/14; Teaching and learning achieving quality for all; First edition, Published in 2014 by the United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization.

2. Ministry of Education and Vocational Training (2012); Basic Statistics in Education in Tanzania (BEST, 2012)

3. Primary Education Development Programme (PEDP III – Final Draft (August 2012); Minister of Education and Vocational Training.

4. Secondary Education Development Programme, SEDP II – Final Draft (July 2010 – June 2015); Minister of Education and Vocational Training

5. Speech by the Ministry of Education and Vocational Training (MOEVT) Hon. Shukuru Kawambwa presenting to Parliament Ministry's expenditure for 2013/14 and budget estimates 2014/15.

6. Speech by the Minister for Finance Hon. Saada Mkuya Salum (MP); introducing to the National Assembly, the Estimates of Government Revenue and Expenditure for 2014/2015 fiscal year.

7. Speech by Minister of State President's Office in charge of Social relations and Coordination Hon. Stephen Masato Wasira (MP), presenting to the National assembly the National Economic Survey for 2013 and Annual Development Plan for 2014/2015.

8. The Annual General report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of the Central Government (MDAs) for the year ended 30thy June 2013.

9. The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Local Government Authorities (LGAs) for the financial year ended 30th June, 2013

10. Tom Hertz, Tamara Jayasundera, Patrizio Piraino, Sibel Selcuk, Nicole Smith, and Alina Verashchagina (2007) "The Inheritance of Educational Inequality: International Comparisons Fifty-Year Trends," *The B.E. Journal of Economic Analysis & Policy*: Vol. 7: Iss. 2 (Advances), (http://www.bepress.com/bejeap/vol7/iss2/art10)

11. Volume II Estimates of Public Expenditure Consolidated Fund Services; Section I and Supply Votes (Ministerial); for the year from July 2014 to June 2015 as presented to the National Assembly

12. Volume III Estimates of Public expenditure, supply votes (Regional) for the year 2014/2015 as submitted to National Assembly

13. Volume IV, Public expenditure Estimates Development Votes; Ministerial and Regional Development Programmes for the year 2014/2015, as submitted to National Assembly

HakiElimu inawawezesha wananchi
kuleta mabadiliko kwenye
elimu na demokrasia

S.L.P. 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu (255 22) 2151852/3 • Nukushi (255 22) 215244
Barua pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org